**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU DIVISHENI YA KAZI**

**DAR ES SALAAM.**

**MAOMBI YA MAREJEO NA.221/2019**

**BAINA YA**

**NISILE MWALUSAMA MCHAPI.......................MLETA MAOMBI**

**NA**

**SALVATION ARMY TANZANIA TERRITORY......MJIBU MAOMBI**

**HUKUMU**

*Tarehe ya mwisho ya Amri:02/03/2021*

*Tarehe ya Hukumu:19/03/2021*

**Z. G. Muruke, J.**

Nisile Mwalusama Mchapi mleta maombi, aliajiriwa na mjibu maombi kama muhasibu wa mradi mnamo tarehe 01/04/2017 kwa mkataba wa mwaka mmoja uliokuwa unaisha tarehe 31/03/2018. Katika mkataba huo walikubaliana kuwa mjibu maombi angemlipia bima ya afya kila mwaka, pia kwa atakayetaka kusitisha mkataba huo, atatoa taarifa ya mwezi mmoja juu ya nia ya kusitisha mkataba huo. Ni madai ya mleta maombi kwamba, aliendelea kufanya kazi hadi tarehe 05/04/2018 alipopewa barua ya taarifa ya kusitisha mkataba wake iliyokuwa imeandikwa tarehe 26/03/2018. Hakuridhika na kuachishwa huko kazi hivyo alipeleka mgogoro wake katika tume ya usuluhishi na uamuzi hapa (CMA) itajulikana kama tume. Uamuzi wa tume ulikuwa upande wa mjibu maombi. Mleta maombi hakuridhishwa na uamuzi huo ndipo alileta maombi haya ya kutengua uamuzi wa tume kutokana na sababu zifuatazo;

i. Muamuzi alikosea kisheria na kwa kushindwa kuzingatia kwamba mleta maombi aliachishwa kazi tarehe 05/04/2018.

ii. Muamuzi alikosea kisheria kwa kushindwa kuzingatia kwamba kitendo cha mjibu maombi kumlipia bima ya afya hadi tarehe 30/03/2019 ni ushahidi kwamba mkataba ulikua ni halali.

Maombi haya yaliungwa mkono na kiapo cha mleta maombi mwenyewe. Katika kupinga maombi haya, mjibu maombi alileta kiapo kinzani kilichoapwa na Avitus Rugakingira ambaye ni wakili wake. Kwa ridhaa ya mahakama shauri hili lilisikilizwa kwa njia ya maandishi. Mleta maombi aliwakilishwa na Denis Mamkwala, muwakilishi binafsi, wakati mjibu maombi aliwakilishwa na wakili Aviatus Rugakingira.

Katika mawasilisho yake muwakilishi wa mleta maombi aliachana na sababu ya pili na kuwasilisha maelezo ya sababu ya kwanza tu. Mwakilishi wa mleta maombi alieleza kwamba, muamuzi ameshindwa kuzingatia ushahidi uliotolewa kwamba mleta maombi aliachishwa kazi tarehe 5/4/2018. Mleta Maombi aliajiriwa kwa mkataba wa mwaka mmoja ambao ulimalizika tarehe 31/03/2018 kama kielelezo P1 (mkataba wa ajira) kinavyoonyesha. Lakini mleta maombi aliendelea kufanya kazi hadi tarehe 5/4/2018 alipopewa barua iliyokuwa imeandikwa tarehe 26/03/2018 (kielelezo P4). Kwa hali hiyo ni wazi kwamba mkataba wao ulihuishwa kwa kitendo cha mleta maombi kuendelea kufanya kazi baada ya muda wa mkataba kuisha. Kama mjibu maombi hakua na nia ya kuhuisha mkataba wao hakua na haja ya kutoa notisi kwasababu mkataba wao ulikuwa umebainisha tarehe ya kumalizika.

Muwakilishi wa mleta maombi alieleza zaidi kwamba, katika barua hiyo ilielezwa kwamba sababu ya kusitisha mkataba huo ni marekebisho ya idara ya fedha na miradi, hivyo kubeba taarifa mbili za marekebisho na kuachishwa kazi. Kwasababu hiyo ni wazi kwamba mjibu maombi alidhamiria kumuachisha kazi mleta maombi bila kufuata taratibu za uachishwaaji kazi kwa sababu ya mahitaji ya kiutendaji(operational requirement) kama ilivyoelekezwa katika kifungu cha 38 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini, Sura ya 366 kama ilivyorekebishwa mwaka 2019) (hapa itajulikana kama Sura ya 366 marejeo ya 2019). Kutokana na hayo mleta maombi alisitishiwa mkataba wake wa pili isivyo halali. Alimalizia kwa kuiomba mahakama itengue uamuzi huo wa tume ili haki ionekane kutendeka.

Kwa upande wake wakili wa mjibu maombi alieleza kwamba, mkataba kati yao ulimalizika tarehe 31/03/2018 kama ilivyoinishwa katika mkataba. Mkataba huo haukuwa na makubaliano ya kuuhuisha, hivyo ulimalizika baada ya kufika muda wake wa ukomo,alirejea Kanuni ya 4(2) ya Sheria ya Ajira na mahusiano(Kanuni za utendaji bora),Gazeti la Serikali Namba 42/2007(Kanuni za utendaji Bora).

Zaidi, wakili Rugakingira alieleza kwamba, mleta maombi ameeleza kwamba aliendelea kufanya kazi hadi tarehe 05/04/2018 alipopokea notisi kuhusu kumalizika kwa mkataba. Hakuna ushahidi wowote uliotolea kuthibitisha kwamba mleta maombi alifanya kazi hadi tarehe hiyo. Aliiomba Mahakama itupilie mbali maombi haya kwa kukosa mashiko.

Baada ya kupitia maelezo kinzani ya wadaawa, mahakama ilikuwa na hoja za kuamua kama ifuatavyo;

i. Endapo mkataba wa wadaawa ulihuishwa?

ii. Nini nafuu za pande zote.

Katika kujibu hoja ya kwanza, ni wazi kwamba mleta maombi aliajiriwa kwa mkataba wa mwaka mmoja ambao muda wake uliisha tarehe 31/03/2018. Ni madai ya mleta maombi kwamba baada ya muda kuisha mkataba huo ulihuishwa kwa sababu aliendelea kufanya kazi hadi tarehe 05/04/2018.

Kanuni ya 4(2)(3) ya Kanuni za Utendaji Bora imeeleza kwamba;

> *4(2) "Where the contract is a fixed term contract, the contract shall terminate automatically when the agreed period expires, unless the contract provided otherwise".*
> *4 (3) "......a fixed term contract may be renewed by default if an employee continues to work after the expiry of the fixed term contract and circumstances warrant it."*

Kwa tafsiri ya Kiswahili ni kwamba, pale ambapo mkataba niwa muda maalum, mkataba utamalizika moja kwa moja pale muda walio kukubaliana unapofika ukomo. Pia mkataba huo utakuwa umehuishwa iwapo muda wake umeisha na muajiriwa akaendekea kufanya kazi na mazingira yanaruhusu hivyo.

Mahakama imepitia kumbukumbu na kuona kwamba zaidi ya barua(kielelezo P4) ambacho hinaonyesha mleta maombi alisaini notisi hiyo tarehe 05/04/2018,hakuna ushahidi mwingine unaothibitisha kwamba mleta maombi aliingia kazini na kufanya majukumu yake toka

tarehe ya kumalizika kwa mkataba huo. Kusaini tu katika barua hii haitoshi kuthibitisha kuwa aliingia kazini baada ya kumalizika kwa mkataba huo. Ni matakwa ya kisheria kwamba yule anaelalamika anapaswa kuthibitisha lalamikao lake.

Pia mleta maombi ameeleza kuwa mjibu maombi alidhamiria kumuachisha kazi kwakua barua hiyo ya notisi imeeleza sababu ya kuachishwa kazi huko kuwa ni marekebisho ya idara ya fedha na miradi. Hivyo aliachishwa kazi kwa mahitaji ya kiuendeshaji bila kufuata taratibu zilizoainishwa katika kifungu cha 38 cha Sura ya 366 marejeo2019. Kwa urahisi wa rejea nina nukuu barua hiyo;

**The Salvation Army**
**Tanzania Territory**

PROJECT OFFICE
P.O. Box 1273
DAR ES SALAAM
TANZANIA
Telephone: +255784831415
+255783364448
E-mail: musamagalgwa@gmail.com

Received: [signature] 5/4/2018

26.03.2018

Nisile Mwasulama
Project Accountant
Tanzania Territory

Dear Nisile Mwasulama

RE: NOTECE OF YOUR CONTRACT AS PROJECT ACCOUNTANT.

As the heading above states I would like to inform you that your Contract will be ending up by 31st March 2018. The decision has been made to not renew your contract as Project Accountant. By this letter we are giving you 30 days as a notice.

The reason is the restructuring of both the Finance Department and the Projects Departments.

Please acknowledge this as an official letter of your contract termination.

Your salary of April 2018 will be paid in full and the end of your contract will be 31.03.2018.

We take this opportunity to thank you all for the great work done and regret for losing such a sincerely and hard working employee.

We will definitely contact you for any suitable profile for you in future. We have your contact details with us. If there is any change with your contact details please let us know.

We wish you all the best for your career.

Yours Sincerely

[signature]
Musa Magaigwa
Major
Project Officer

THE SALVATION ARMY
TANZANIA TERRITORY
26 MAR 2018
Territorial Finance Council
TANZANIA TERRITORY

"FORWARD TOGETHER"

Ukiangalia aya ya kwanza ya barua hii, iko wazi kabisa kwamba mkataba huu utaisha tarehe 31/03/2018 na muajiri alieleza wazi nia ya kutohuisha mkataba wao baada ya kumalizika. Na sababu ya kutohuisha mkataba huo ni marekebisho katika idara za fedha na miradi. Lakini mleta maombi kwa matakwa yake binafsi alichagua kutoona aya ya kwanza na ku ng'ang'ana na aya ya pili ya sababu. Kama ambavyo tume imeamua, ni dhahiri kwamba mkataba huo haukuhuishwa kama anavyodai mleta maombi.

Katika hoja ya pili, baada ya kuamua kuwa hakukuwa na kuhuishwa kwa mkataba, ni dhahiri kwamba stahiki alizonazo mleta maombi ni malipo ya notisi na cheti cha utumishi, ambavyo hakun a ubishi kwamba alikwisha lipwa. Minajili hiyo basi, mahakama hii haioni sababu ya msingi ya kutengua uamuzi wa tume.

Kwa mazingira hayo, maombi haya yanatupiliwa mbali kwa kukosa mashiko.Uamuzi wa tume umethibitishwa. Imeamriwa hivyo.

Z. G. Muruke

**JAJI**

19/03/2021

Uamuzi huu umesomwa mbele ya mleta maombi mwenyewe na Avitus Rukakingira, Wakili wa mjibu maombi.

Z. G. Muruke

**JAJI**

19/03/2021

Mahakama ya Kazi Tz